

# Haruna Na mpira wake

## Swahili

Haruna anapenda sana kucheza mpira. Anao mpira mmoja mzuri sana. Aliupata kwenye sikukuu yake ya kuzaliwa na huo mpira ni mwekundu na mweupe.

Siku moja asubuhi Haruna aliamua kwenda nje kwenye bustani na kuchezea mpira wake. Baada ya kuvaa nguo, kunywa chai na kupiga mswaki alienda kuchukua mpira wake.

Lakini mpira haukuonekana!

Haruna alidhani kuwa labda mpira utakuwa ndani ya kikapu. Aliangalia lakini mpira haukuwepo.

Alirudi sebleni na kuangalia chini ya kiti lakini haukuwepo.

Sasa Haruna aliweza kufikiria sehemu moja tu ambapo mpira ungekuwepo - juu ya kabati. Alipanda juu ya kiti na kuangalia juu ya kabati lakini mpira haukuwepo.

Haruna alianza kusikia huzuni kwasababu alishindwa kuupata mpira wake. Lakini huku akiwaza alisikia sauti ya baba yake ikimuita kutoka nje.

Alikimbilia nje upesi na kumuona baba yake ameushika mpira wake mwekundu na mweupe.

Baba yake Haruna pia alipenda sana kucheza mpira na kwa pamoja walicheza siku nzima.

# Haruna Na mpira wake

## English

Haruna loves playing football. He has one really nice ball. He got it on his birthday and the ball is red and white.

One morning Haruna decided to go out into the garden to play with his ball. After getting dressed, drinking tea (having breakfast) and brushing his teeth he went to collect his ball.

But the ball was no-where to be seen!

Haruna thought that maybe the ball is inside the basket. He looked but the ball was not there.

He went back into the livingroom and looked under the chair but it wasn't there.

Now Haruna could only think of one more place where the ball might be – on top of the cupboard. He climbed on to the chair and looked on top of the cupboard but the ball was not there.

Haruna started feeling sad because he could not find his ball. But while he was thinking he heard his dad's voice calling him from outside.

He ran outside quickly and saw his dad holding his red and white ball.

Haruna's dad also liked playing football and they played together the whole day.